# *MADHIHIRISHO*

Pamoja na shuhuda hizi na rambirambi za dada yetu aliyetuacha, ningetaka kuacha maneno haya, pia. Kufahamiana kwangu mara ya kwanza na familia ya Bell kulikuwa ni mumewe, Jimmy, ambaye alikuwa rafiki msiri wa baba yangu ambaye ametuacha. Ndipo miaka kadhaa baadaye, nikawa mhudumu nami nikafahamiana na Dada Bell, na kumjua kama Mkristo mwaminifu kweli. Sote tutamkosa, kila mahali. Ni rahisi sana kusema maneno juu ya mtu kama huyu, kwa sababu haikubidi kuficha lolote. Yeye alikuwa kile kilichohitajika kuwa Mkristo.

2 Nilipomsikia huyu dada akiimba, dakika chache zilizopita, ilinikumbusha tu sana juu ya kuimba kwake, kama tumjuavyo mahali hapa. Alipenda kuimba. Nina furaha sana kwamba hili lilifanywa, kwa kuwa ilionyesha kweli jinsi Dada Bell angalijisikia. Yeye angetaka kujieleza kwa njia hiyo. Maombi yangu, na maombi maaminifu ni, kwamba sote tutaufikia mwisho wa safari tukiwa na ushuhuda kama aliokuwa nao.

3 Ningependa kusoma baadhi ya Maandiko hapa, sehemu moja tu. Ninahisi kwamba yeye alikuwa mwenye kulipenda sana Neno la Mungu, nalo Neno Lake ni la Milele sana. Nami nilifikiri ningesoma sehemu moja ya mlango wa 14 wa—wa Ayubu.

> *Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke, siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu.*
>
> *Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa: hukimbia kama kivuli, wala hakai kamwe.*
>
> . . .nawe *wafumbua macho yako kumwangalia mtu kama yeye, na kunitia katika hukumu pamoja nawe?*
>
> *Ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi kitoke katika kitu kichafu? Hapana awezaye.*
>
> *Kwa kuwa siku zake zimeamriwa, hesabu ya miezi yake unayo wewe, Nawe umemwekea* yeye *mipaka yake asiyoweza kuipita;*
>
> *Acha kumwangalia yeye, apate kupumzika, hata* akiisha kutimiza *siku yake, kama aliyeajiriwa.*
>
> *Kwani yako matumaini ya mti, ya kuwa ukikatwa utachipuka tena, wala* matawi *yake hayatakoma.*
>
> *Ijapokuwa mizizi yake huchakaa mchangani, na shina lake* kufa *katika udongo;*
>
> *Lakini kwa harufu ya maji utachipuka, na kutoa. . . kama mche.*

*Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia: naam,. . . hutoa roho, naye yupo wapi?*

*Kama vile maji kupwa katika bahari, na* mafuriko kupunguka *na* kukauka*:*

*Ni vivyo hivyo mwanadamu hulala chini, wala* hainuki*: hata wakati mbingu kutokuwako tena, hawataamka, wala* waamshwe *usingizini mwao.*

*Laiti* ungelinificha *kuzimuni, ukanilinda kwa siri, hata* siku za *gahadhabu zako zitakapotimia,. . .*

*Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena? Mimi ningengoja siku zote za vita vyangu, hata kufunguliwa kwangu kunikifikilie.* Mimi . . .

*Wewe ungeita,. . .ningekujibu:* utakuwa *na tamaa* kufanya *kazi ya* mkono *wako.*

*Lakini sasa wazihesabu hatua zangu:. . .*wewe *huchungulii dhambi yangu?*

4 Tukisoma kutoka kwenye Neno la Milele, ningetaka tuwazie juu ya neno moja tu kwa dakika chache, nalo neno hilo ni: *Madhihirisho.*

5 Kuna mengi sana ya maisha ambayo ni madhihirisho. Na hakuna mtu anayeishi duniani ila ambaye wakati fulani maishani mwake hana budi kusimama na kuwazia anakotoka, ni nini kusudi lake hapa, na anakoelekea baada ya hapa. Kila mtu anapenda, angetaka kuangalia kupita pazia.

6 Tukisoma hapa kutoka kwenye Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia, Ayubu, huyu mzee wetu, yeye alikuwa akijaribu kujua kitu kiki hiki. Naye alikuwa akitoa shauku yake ya Mungu, akielezea kwamba Yeye alikuwa ni u—uzima baada ya mauti.

7 Wakati mwingine tunajisikia kwamba, tunapokabiliwa na kitu kama hiki, kwamba hiki ndicho chote. Bali sivyo. Ni kule kubadilishwa. Ni ninii . . . hatua moja juu zaidi. Ni kupita kutoka kwenye maisha mamoja hadi mengine.

8 Naye Ayubu, nabii, wakati alipokuwa akiyawazia mambo haya, aliyagundua katika uhai wa mimea, maisha ya mimea, uhai wa mti. Kwa hiyo alikuwa akiona ya kwamba, jinsi ambavyo hapana shaka Mungu yuko katika maumbile Yake; kwamba kama Yeye aliumba maumbile, basi hana budi kuishi katika hayo maumbile, kwa sababu aliyaumba kwa kusudi fulani, ili aweze kuishi mle Mwenyewe, kama nyumba ambayo mtu angeijenga. Maskini uhai huu mdogo sana ulio ndani ya viumbe wote wa Mungu umetiishwa kwa Muumba wake. Naye alikuwa akiwazia, kwamba, kama dhoruba ikija na ingeuangusha mti mkubwa mno, hata hivyo, huo haukuwa ndio mwisho wa mti huo. Ungeishi tena. Kama huo mti ulikufa, ungeishi.

9 Na mara nyingi, wakati tunapochanganyikiwa, kama tungeangalia tu kote kutuzunguka, unaweza kumwona Mungu kila mahali. Sasa tutamchukua Yeye, kama vile katika mti, kama huo mti ukiwekwa hapa.

10 Na kila kitu kipo hapa kutumikia kusudi fulani, kama tu vile tulivyo hapa kutumikia kusudi fulani, kama tu vile dada yetu alivyokuwa hapa kutumikia kusudi fulani. Sote tupo hapa kwa kusudi la Mungu, ikiwa tunaweza kujua hilo kusudi ni lipi na kisha tulitumikie vizuri. Hapo, hakika, kama Mungu anajali vya kutosha juu ya ufufuo wa uhai wa mimea, Yeye anajali vya kutosha juu ya ufufuo wa uhai wa mwanadamu.

11 Kwa hiyo Ayubu aliona, yule mzee wetu, ya kwamba—ya kwamba mti, kama ulikufa, uliishi tena. Na jinsi ambavyo msimu wa kiangazi na wa baridi kali ulivyobadilisha asili yake, na kila siku ikaacha ushuhuda. Yeye aliona kama m—mti ulikuwa ukiishi katika msimu wa kiangazi, na inaonekana kana kwamba wakati wa baridi kali ulikufa, yale majani yaliyoning'inia juu ya huo mti.

12 Sasa, tunafundishwa katika Maandiko, ya kwamba, kuna Mti wa Uzima. Ulikuwa katika bustani ya Edeni. Nao Mti huu wa Uzima ndipo Wakristo wanaponing'inia, kama jani kwenye Mti huu.

13 Na sasa katika wakati wa baridi kali, wakati hayo majani yanapendeza, mbona, hayo . . . Ama, katika wakati wa kiangazi, hasa, wakati hayo majani yanapendeza na ni ya kijani kibichi, baada ya kitambo kidogo jalidi inakuja na kuyatia rangi tofauti, nayo yanapukutika kutoka mtini. Nao uhai unarudi katika mzizi wa huo mti. Kama tukiangalia tu, ni jambo la kisiri.

14 Hapa wakati fulani uliopita, nilikabiliwa, kuzungumza na mtu aliyedai kwamba ni kafiri, asiyeamini. Nasi tulikuwa tumesimama karibu na mtofaa uliokuwa ni mali yake. Ndipo nikamwuliza huo mti ulikuwa na umri gani, naye akaniambia miaka kadhaa, na kwamba ni pishi ngapi za matofaa ulizotoa kila mwaka. Na hii ilikuwa ni sehemu ya mwanzoni mwa Agosti, nami nilijua, niliona hayo matofaa tayari yalikuwa yakianguka, nayo majani yalikuwa yakigeuka kuwa hudhurungi. Basi nikamwambia, "Ningetaka kukuuliza swali." Nikasema, "Ni kwa nini hayo majani yanageuka kuwa hudhurungi na kuanguka kutoka mtini kabla jalidi yoyote kuyagusa?"

15 "Vema," akasema, "ni baridi kali inakuja. Na sababu ya kugeuka hudhurungi ni kwa kuwa uhai umeliacha jani."

Nikasema, "Kwani uhai huo ulienda wapi?"

16 Naye akaniambia, "Umerudi kwenye mzizi wa mti, mahali ulipotoka."

Nami nikasema, "Huo ndio mwisho wa hilo jani?"

17 Akasema, “La. Uhai huo utarudi tena kwenye msimu ujao wa kuchipusha majani, ukiwa na jani jipya.” Kamwe hakuwa ameona hilo hapo awali.

18 Nikasema, “Basi, naomba uniambie, bwana, ni Akili gani inayolitoa jani hilo kutoka mtini hata kabla ya majira ya baridi, na kuurudisha uhai wake chini ardhini, kwa ajili ya usalama, mpaka kuja kwa msimu mwingine. Ungeweza kuweka maji katika ndoo na kuyaweka juu ya nguzo, kamwe hayatabadilika kwa msimu. Kwa hiyo inaonyesha kwamba kuna Mungu Ambaye huutawala uhai.”

19 Nasi ambao tunadai kuwa Wakristo, tuliozaliwa kwa Roho wa Mungu, tumekuwa, kwa neema ya Mungu, tumehamishwa kutoka kwenye mti wa mauti hadi kwenye mti wa Uzima. Basi wakati moja la hayo majani linapoanguka chini, kama nilivyosikia ushuhuda ule kutoka kwa ninii . . . kanisa hili zuri sana, kwenye kanisa la Kibaptisti la Gilt Edge, ambamo wengi wa marafiki zangu wa thamani ni washiriki, ambako moja ya majani yake limeanguka. Tunajua ya kwamba uhai huo umemrudia Mungu Yule aliyeutoa kwa ajili ya kusudi fulani, upate tu kuja tena katika ufufuo wa kiama; kamwe usianguke tena, katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Ule wakati mkuu unakuja.

20 Ayubu alikuwa ameyaona mambo haya. Kisha akaona katika maisha ya jua.

21 Kama mtatazama, mnamo asubuhi, jua huchomoza, ni mtoto mchanga. Miali yake ni dhaifu. Halafu linafikia utineja wake, yapata saa tatu ama saa nne. Ndipo adhuhuri, katikati ya mchana, liko kwenye nguvu zake. Kisha linaanza kushuka, na hatimaye linatua tena huko Magharibi, wakati linapokufa kwa siku hiyo. Tungeweza kuita huo mwisho wa hilo jua? La. Kesho yake asubuhi, huchomoza tena, kutuletea siku mpya.

22 Sasa, ni kitu gani hiki? Ni madhihirisho ya Mungu. Nalo neno *dhihirisho* linamaanisha “kufanya hisia ijulikane.” Ni udhahiri wa Mungu . . . dhihirisho kwetu, kutufanya tujue hisia Yake kutuhusu sisi, kwamba mauti hayatutenganishi Milele. Tutafufuka tena, tutarudi tena.

23 Kila wakati mbegu inapokufa ardhini, katika msimu wa majani kupukutika mwakani, kama tu vile maua haya, hayo, maskini hizo mbegu ndogo huanguka kutoka kwayo wakati jalidi inapozipiga, nayo mbegu inaingia ardhini. Na kadiri linavyoweza kuonekana la kigeni, hata hivyo ni kweli, Mungu ni asiye na kikomo sana hivi kwamba Yeye hapuuzi chochote. Yeye ana msafara wa mazishi kwa ajili ya ua Lake. Baada ya jalidi kuyapiga, ndipo huja mvua ya msimu wa majani kupukutika, na machozi makubwa mno, ya matone ya mvua, hushuka kutoka mbinguni, na kuizika hiyo mbegu ya ua, yanaipigapiga, na labda inaingia inchi moja ama mbili chini ya ardhi. Ndipo upepo

baridi wa kipupwe unaanza kuvuma, na—nazo hizo petali ndogo zimekwisha, na shina limekwisha, halafu basi tunguu linaganda na kukauka. Kisha maskini mbegu hiyo inaganda, halafu nyama yake inatoka. Na, mbona, ifikapo wakati wa kuchipusha, huwezi kupata chochote kilichosalia kwake.

24 Lakini huo ndio mwisho wa hilo ua? La hasha. Liliwekwa hapa kwa kusudi fulani. Basi wakati limetimiza kusudi lake vizuri, ndipo Mungu anatujulisha, kwa hilo ua, dhihirisho Lake kwetu.

25 Kwa hakika tu kama vile jua linavyoikaribia dunia kidogo zaidi, kuleta mwali wenye joto zaidi kidogo, usingeweza kuuficha uhai huo popote. Ungeweza kuufunika kwa jiwe. Hivi ulipata kuona unapoweka saruji yako wakati wa baridi kali, ni wapi nyasi imeshikana sana katika msimu wa kuchipusha? Moja kwa moja nchani mwa hiyo saruji. Mbona hivyo? Ni uhai huo ulioko chini ya hilo jiwe. Jua linapoanza kuiangazia ardhi, huwezi kuuzuia uhai. Utapenya utoke chini ya hiyo saruji na kuchomoza kichwa chake juu, kumsifu Mungu, kwa sababu jua ndilo ufufuo. J-u-a ndilo ufufuo wa uhai wote wa mimea. Huwezi kuuficha mradi tu jua linawaka.

26 M-w-a-n-a anaonekana kuwa, mara nyingi, mbali sana. Lakini Yeye anapoanza kumulika, "Jua la haki litawazukia likiwa na uponyaji katika mbawa Zake." Ndipo kila uhai, haidhuru umezikwa wapi, kwa kilindi jinsi gani, umbali gani majini, ama katika mchanga, penye mawe, utafufuka kwa utukufu wa Mungu.

27 Kwa sababu, Mungu anatuelezea, akituonyesha kile tu Yeye anachofanya. Kusudi Lake ni kutuonyesha, kupitia kwa maua, kupitia kwa jua, kupitia kwa miti, kupitia kwa uhai wote, kwamba Yeye ndiye ufufuo na Uzima. Mungu huufufua Uhai Wake unapotumikia kusudi Lake.

28 Basi kama ua linatumikia kusudi lake, naye Mungu ana ufufuo kwa ajili ya hilo ua, ni zaidi sana vipi kwa dada yetu ambaye anatumikia kusudi lake maishani. Mungu anao ufufuo kwa wale wanaotumikia kusudi lao. Tunaweza kujua kusudi letu na kisha tulitimize.

29 Maskini maua haya madogo, huenda mkauliza juu yao. Yapo hapa, alasiri ya leo, kutumikia kusudi fulani. Hilo ndilo maua haya, Mungu aliloyakusudia, kutumikia kusudi fulani. Lingeweza kuendelea zaidi na zaidi.

30 Mkitazama, maua haya yote si ya rangi moja ya maua. Yanatofautiana katika rangi, ikionyesha ya kwamba Mungu ni Mungu wa vitu vya namna nyingi. Yeye anapenda rangi mbalimbali. Kuyachanganya pamoja hufanya shada ambalo Yeye anapenda. Mungu, Mungu wa vitu vya namna nyingi. Yuna maua Yake meupe. Yuna maua Yake mekundu. Na ninii

Yake, rangi zote za maua, na kuyaweka pamoja hutumikia kusudi Lake.

31 Anayo milima mikubwa, na vilima vidogo, na nyanda. Anayo majangwa. Anayo bahari. Anao mwaloni, mtende. Kila kitu kikipatana pamoja mahali pake, ambapo, Mungu, yule Mungu wa maumbile yote anaweza kuishi na kufurahia utu Wake, kama kuishi katika viumbe Vyake katika wakati, wanaotimiza kusudi Lake.

32 Kama Yeye anawazia vya kutosha kuyafufua hayo, na alifanya njia ya kuepukia kwa hayo, kwa ajili ya utumishi katika siku za usoni tena, ni zaidi sana vipi anavyowazia juu ya watu, haijalishi sisi ni kina nani, ni wa jamii gani, rangi, kanuni ya imani, ama chochote zaidi, ambao tunaweza kuishi pamoja katika umoja wa Uwepo wa Mungu na baraka Yake. Kutakuwako na ufufuo, siku moja, hakika tu kama kulivyo na ufufuo wa ua. Sote tunaona hayo. Sote tunaamini hayo. Sote tunajua ya kwamba vitu hivi vyote ni madhihirisho. Vinashuhudia, vikitwambia, vikifanya, kujua hisia ambayo Mungu anatutaka tujue.

33 Watu walioyatuma maua haya, marafiki wa dada yetu walioyatuma maua haya, wao pia wanaijulisha familia, wakiwaonyesha hisia yao ya huruma ya rafiki, ya dada, ama—ama mpendwa. Wanajaribu kudhirihisha. Ni madhihirisho, kujulisha, kutangaza jambo fulani.

34 Mambo haya yote ambayo tungeweza kuzungumzia, kwa saa nyingi, madhihirisho ya Mungu kwa jamii ya mwanadamu, yote haya yana sehemu yao, nayo yanaitumikia vizuri. Kila ua, kila mti, kila kuchomoza kwa jua, kila kutua kwa jua, kila kitu hutumikia sehemu yake vizuri. Lakini madhihirisho hayo yote ya Mungu, akitujulisha sisi, na kutupa mfano, kwamba Yeye anaenda kufanya dhihirisho kuu siku moja, dhihirisho la Milele.

35 Ndipo akatutumia chapa ya sura Yake, katika mfano wa Mwana Wake. Mungu alimtuma Mwana Wake, katika chapa ya sura Yake Mwenyewe, kuitangazia jamii ya mwanadamu yale Yeye aliyotuwazia sisi. Alibadilisha sura Yake. Akawa mwanadamu. Akawa mmoja wetu.

36 Kutoka kwa Mungu, Baba wa Milele, kutoka kwa Muumba mkuu Ambaye, kabla ulimwengu haujakuwapo, alililijaza anga lote, wakati. Hapakuwapo hata na ki—kimondo ama kimondo cha nuru, wala hapakuwapo na atomi wala molekuli, Yeye angali alikuwa ni Mungu. Na Yeye daima atakuwa Mungu. Lakini Yule mkuu Ambaye. . . Kama ungeweza kuangalia juu usiku na kuona nyota kwenye mfumo wa jua. Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa na majaliwa ya kuangalia kupitia darubini hii kubwa, na ambapo wanadai ungeweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru, vimondo vya nuru. Na kupita hiyo

kungali kuna miezi na nyota na ulimwengu mwingi, ambao Yeye hudhibiti.

37 Halafu basi Yeye alijali sana vya kutosha kufanya dhihirisho kwetu, akijua kwamba Yeye ni mkuu sana. Hata hivyo, Yeye alishuka katika mfano wa mwanadamu, kuonyesha kile Yeye alichokuwa. Akafanyika Mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko. Aliishi maisha ya binadamu. Hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Yeye alikuwa akionyesha kile Kilicho, kile Mungu alichokuwa. Aliwaponya wagonjwa wetu tulipokuwa wagonjwa. Aliwafufua wafu, kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni chapa ya Mungu. Alituwekea mpango sisi sote, ambapo sisi pia tungeweza kuangalia dhihirisho hili dogo na kumwona Mungu. Ndipo tungeweza kuangalia juu na kuona dhihirisho kuu la Mungu, na kuwa na hakikisho, basi, ya kwamba wasaa huu utakapokuja, huu sio mwisho wake.

38 Ninapenda kauli ambayo dada yetu, katika kuimba, aliisema dakika chache zilizopita, "Huyu ni dada yangu. Nisingeweza kuuimba jinsi hii isipokuwa yeye alijua mahali alipokuwa." Mnaona?

39 Ipo njia ambapo tunajua mahali tunakoelekea, kwa sababu chapa ya nafsi ya Mungu iliuweka mpango huu. Pia, Yeye alisema, kila atakayeukubali mpango huu angekuwa na Uzima wa Milele. Yohana 5:24 ilisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

40 Dhihirisho kuu kuliko yote lilikuwa ni Yesu Kristo, Yule aliyetufanyia njia. Alitimiza na kuthibitisha madhihirisho yote ambayo maua haya, na uhai wa mimea, na kadhalika, na jua, na mfumo wa jua, vimeshuhudia kabla ya Kuja Kwake, ya kwamba alikuwa anakuja Mwenye Haki ambaye angetufanya tuliamini kwa uthabiti, kwa sababu Yeye angekuwa ni chapa ya Mungu iliyodhihirishwa. Basi Yeye alipokuja, na kufanya yale aliyofanya, alithibitisha kwamba madhihirisho haya yalikuwa sahihi. Akayathibitisha. Kwa sababu, kama vile ua linavyofufuka tena, mti unavyofufuka tena, jua linavyofufuka tena, vivyo hivyo Mkristo atafufuka tena. Haina budi kuwa hivyo. Kwa sababu, Mungu, katika chapa iliyodhihirishwa ya mwanadamu, ama mwanadamu akiwa katika chapa ya Mungu iliyodhihirishwa, alilithibitisha kwa ufufuo Wake.

41 Basi, mle ndani, nabii alipoyaona mambo haya yakitendeka; Ayubu, hapo alipoona uhai wote wa mimea, na kadhalika. Basi, sisi tunaoifahamu Biblia tunajua hilo. Akiketi kwenye lundo hili la majivu, katika dhiki, matatizo yalikuwa yamempata. Wafuasi wake wa kanisa walikuwa wamemwambia ya kwamba yeye alikuwa ninii . . . alikuwa ametenda dhambi kisiri.

42 Mara nyingi imesemwa, kwamba, "Mtu hufa kabla ya wakati wake, ama kitu fulani, kwamba labda ni dhambi fulani waliyotenda. Walifanya kosa fulani." Hapana . . . Sivyo ilivyo kwa Mkristo.

43 Wakati yeye alipoona dhihirisho hili kuu, la mwisho, Mungu akitambulisha mpango Wake kupitia Yesu Kristo, yeye alilia kwa sauti. Hapo radi zilipomulika na ngurumo zikanguruma, yeye alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili wangu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mimi mwenyewe." Yeye aliona hilo dhihirisho la mwisho, mamia mengi ya miaka kimbele. Lakini, akiwa ni nabii, katika ono yeye aliona kuja kwa dhihirisho kuu la Mungu.

44 Angeweza kuangalia chini na kuona ufufuo wa mbegu. Angeweza kuona ufufuo wa miti. Na ufufuo wa jua, likiisha kutimiza wakati wake, na kufufuka tena; likatumika kwa siku moja, likafufuka kwa ajili ya siku nyingine. Maua kwa ajili ya ibada moja ya mazishi, hufa, kisha yakafufuka kwa ajili ya ibada ya mazishi ya mtu mwingine. Kila kitu kikitumikia kusudi lake. Kisha akaona, huko mbali, Kuja kwa yule Mwenye Haki, ndipo akapaza sauti, "Ninajua ya kuwa Mkombozi wangu yu hai."

45 "Mwili wangu utakaa katika tumaini," akasema Daudi, "kwa sababu Yeye hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu; wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu." Yeye aliiona siku hiyo, ule udhihirisho mkamilifu wa Mungu, yale Yeye atakayofanya; kumjulisha, mwanadamu, kwamba mauti siyo mwisho wa safari.

46 Huu sio mwisho. Huu ni mwanzo. Ni mwisho wa huzuni. Ni mwisho wa wakati wa maamuzi. Lakini ni mwanzo wa wakati wa furaha na thawabu. Sio mwisho wa kila kitu. Ni mwisho tu wa—wa vitu vipatikanavyo na mauti, kuanzisha kitu kisichopatikana na mauti. Ameenda kwa raha yake. Mungu aipe raha nafsi yake.

47 Sasa, yeye alililia dhihirisho hili kuu, kwa sababu aliona kilichokuwa kinaenda kutukia.

48 Sasa hebu tuufikie uamuzi huu. Tumekusanyika hapa leo hii, ku—kuonyesha, au kufanya ijulikane hisia yetu kuhusu jirani, kuhusu dada, kuhusu mke, kuhusu mama. Hiyo ndiyo sababu tumekusanyika alasiri ya leo; kufanya ijulikane, kuonyesha hisia zetu, msiba wetu. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa, kufanya jambo hili. Huyu baba kuonyesha kumpoteza mke wake; watoto, mama; jirani, ama dada.

49 Sisi wahudumu. Kama nilivyowasikia, kote humu jengoni, wakitoa hayo matamshi ya ajabu, mazuri sana, ya kufariji, dhahiri, kile huyu dada alikuwa amemaanisha kwao, na katika kusanyiko lao. Sisi wahudumu tumekuja, alasiri ya leo. Hakika,

mioyoni mwetu, tunasikia huzuni, pia. Lakini tumekuja kufanya ujulikane udhihirisho wa Mungu, pia, Ukweli Wake kuhusu jambo hili lote. Tumekuja kuonyesha yale Mungu asemayo kulihusu, kuifariji mioyo ya watu; kuwajulisha, kadiri mshtuko huu uwezavyo kuwa ni mkubwa, hata hivyo uko katika majaliwa ya Mwenyezi Mungu kulifanya jinsi hii, nao ni mpango Wake. Wala huu sio mwisho. Huu ni mwanzo wa maisha mapya.

50 Kisha sisi ambao Mungu hutufundisha katika Neno Lake, kuhusu mambo haya, tumekuja kutoa udhihirisho wetu. Na jinsi nilivyo na furaha juu ya huyu alasiri ya leo, kwamba sisi sote tunaweza kuonyesha jambo lile lile kwenye Neno la Mungu, kwa sababu yeye alilitimiza Hilo.

51 Dada Bell, kama tulivyomfahamu hapa maskanini, mwanamke Mkristo, mtakatifu, wa kupendeza, alifanya madhihirisho yake, pia. Alifanya zijulikane hisia zake kuhusu Mungu. Kama nilivyosikia tanzia ikisomwa, muda mfupi uliopita, hata kabla Ndugu Jim hajamwoa, nadhani, huko chini Tennessee, yeye alifanya uamuzi wake. Alifanya dhihirisho lake. Kwa hiyo, ni shuhuda. Na kadiri nijuavyo mimi, tangu siku hiyo na kuendelea, kamwe hajaacha kufanya udhihirisho huo. Labda, leo hii, kama ilivyo kwenye ushoroba wa Mbinguni, mahali fulani huko katika milki za Milele za Utukufu, akitembea kwenye barabara za Mungu, angali akiyadhihirisha. Kupita vivuli hivi vya milki ipatikanayo na mauti, angali anayadhihirisha.

52 Dada Bell, tunavyomfahamu, hakuuonea aibu ushuhuda wake. Si hata wakati mmoja aliuonea haya ushuhuda wake. Si hata wakati mmoja alisita kusema jambo fulani. Alilionyesha, wala hakuona aibu. Jinsi ambavyo nimemwona akisimama huko nyuma huku ameinua mikono yake hewani, na machozi yakitiririka mashavuni mwake. Nikamwona amesimama hapa kwenye mimbara hii, na kuimba nyimbo ambazo zingelifanya kanisa zima liingie katika shangwe, za Nchi, iliyo mbali sana na hapa. Hakuona aibu. Yeye alitoa ushuhuda wake kila mahali. Kila jirani, kila kanisa, popote alipokuwa ameshirikishwa, alijifanya ajulikane, akaelezea yale aliyowazia kumhusu Mungu. Yalikuwa ni maisha yake, yote yale angaliweza kuwa, alielezea kile alichokuwa katika Kristo Yesu, kiumbe kilichozaliwa upya.

53 Alikuwa ni rafiki mpendwa wa maskini mama yangu mpendwa ambaye—ambaye alipanda vipandio vile vile, majuma machache yaliyopita. Leo hii, wako pamoja.

54 Ni jambo zuri jinsi gani, kuona madhihirisho, jinsi Mungu afanyavyo. Barua zake; Dada Bell. Kila wakati ningekuja nyumbani, Billy, mwanangu, angeniletea lundo la barua, wito wa simu, sikuzote, kutoka kwa Dada Bell. "Mwombee *huyu*. Mwombee *yule*." Hilo, lilikuwa likifanya nini? Kwangu mimi, huo ni udhihirisho wake, akitambulisha kilichokuwa ndani

yake; mzigo kwa ajili ya mwanadamu mwenzake, mzigo kwa ajili ya watoto wake, mzigo kwa ajili ya kila mtu aliyekuwa karibu, na kila mgonjwa.

55 Dada Bell karibu aliishi kwa neema ya Mungu, hii miaka michache ya mwisho. Alikuwa ni mwaminio mwaminifu katika nguvu za Mungu za uponyaji. Basi ilitokea hivi majuzi usiku . . . Kamwe maishani mwangu sijapata kumwombea, na kuomba pamoja na maskini mtakatifu huyo mpendwa, mpaka, isipokuwa Mungu alimponya.

56 Ndipo hivi majuzi usiku, nilipopigiwa simu, ndio kwanza niingie kutoka Arizona, karibu yapata usiku wa manane. Walimpigia mwanangu simu na kusema, "Dada Shepherd, rafiki ya Dada Bell, anakutaka umwombee. Yuko hospitalini." Nilifahamu kwamba ni Dada Shepherd; mama fulani, labda yumo humu jengoni sasa, jina lake Shepherd, ambaye alimfahamu. Nilidhani alikuwa hospitalini.

57 Kesho yake asubuhi wakapiga simu tena, yapata saa tano na kitu, na kusema, "Si Dada Shepherd. Ni Dada Bell, mwenyewe, yuko hospitalini." Basi kuona hayo, majaliwa ya hekima na mpango wa Mungu. Kabla kamwe hajaweza kufika kule, Dada Bell alikuwa tayari amepanda vile Vipandio vya dhahabu. Kabla sijaweza kufika kule, Mungu alikuwa tayari amelichuma waridi Lake la rangi, apate kufanya shada Lake kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Kabla sijaweza kufika kule, alikuwa ameenda kukutana na Mungu. Dhihirisho la Mungu la upendo Wake!

58 Miaka hii yote ya ndoa yenye furaha ilikuwa ni dhihirisho la uaminifu wake kama mke, kufanya makazi kwa ajili ya mume wake na watoto wake. Huo ulijidhihirisha kupitia nyakati ngumu, wakati jamaa wadogo wakiwa wamezunguka mezani, na mazingira magumu. Na, mama, inahitaji mama kujua jinsi ya kujumuisha vitu pamoja, kuvifanya vidumu—vidumu, wakati maskini midomo yenye njaa imeizunguka meza. Lakini, kusimama karibu na mumewe, mwaminifu, kusimama karibu na watoto wake, ilikuwa ni dhihirisho la uaminifu halisi. Hiyo ni mbele ya kila mmoja wenu. Isingenipasa kusema hilo. Mnajua hilo kuwa ni kweli. Mnaona? Naam, bwana.

59 Na maombi yake yasiyoshindwa kwa ajili ya watoto wake! Siamini niliwahi kukutana naye, ama kumwacha, pasipo yeye kuomba haja kwa ajili ya watoto hao. Hiyo ilionyesha umama halisi, tukijua ya kwamba maisha ni ndoto tu ama mahali pa kufanyia maandalizi. Kwa ajili ya watoto wake, alitaka kukutana nao katika Nchi iliyo ng'ambo ya hapa, ambako hakutakuwako na nyakati ngumu tena. Sikuzote angeniambia . . . Yeye aliniita Ndugu Billy. Angesema, "Ndugu Billy, waombee watoto wangu, asije akapotea mmoja wao." Kama hilo si dhihirisho la umama halisi; mama anayewajali

watoto wake, anayejali jirani zake, mume wake, mpendwa wake! Ni Mungu katika huyo mwanamke, akionyesha mambo ya Milele.

60 Jinsi ninavyomhurumia mumewe, rafiki yangu mwema. Jinsi ninavyowahurumia hao wavulana, kusikia ujumbe wa baadhi yao huko Ujerumani na mahali mbalimbali, mama amewaacha. Lakini huenda ameondoka mbele zenu hapa, enyi wavulana, bali ha—hajafa. Yu hai milele. Yeye yu hai katika Nchi ambamo aliomba ya kwamba kila mmoja wenu angekutana na yeye. Msiache audhike. Nina hakika hataudhika.

61 Ninaona njukuti moja imetoka kwenye gurudumu hilo, alasiri ya leo. Nakumbuka wakati njukuti ya kwanza ilipotolewa kwenye familia yangu. Moja moja, zitaanguka. Haitachukua muda mrefu mno. Sikilizeni. Gurudumu hilo linaweza kuunganishwa tena, katika Nchi nyingine ambako hakuna magurudumu yaliyovunjika, ambako uchumi mkuu wa Mungu unaweza kupatikana na unaweza kubingirika kote katika nyakati. Na iwe hivyo, enyi familia. Sikuzote mmekuwa na mama; sasa mwe pamoja naye milele. Hiyo ni kweli.

62 Jambo lingine lililodhihirisha upendo wa Mungu. Kama ninavyosikia, kwamba, ombi lake lilikuwa kwamba kamwe hatakuwa mkongwe na kukawia sana, imbidi kukawia na kubebwabebwa uzeeni, na kupooza na—na kuugua mara kwa mara, na huku yuafa polepole. Mungu alijibu ombi hilo. Hiyo ni kweli. Mbona, Jumapili kadhaa tu zilizopita, alikuwa amesimama hapa kwenye benchi la kanisa, akiimba Injili tukufu ya Kristo.

63 Ni kitu gani hiki? Ni kitu gani hiki cha mama, ilionekana kana kwamba, ni kuondoka kabla ya wakati, yapata miaka sitini na mitano, kuondoka? Hilo linamaanisha nini? Ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe, kwamba, "Hatawanyima kitu kizuri hao watakaotembea sawa mbele Zake." Mungu, akionyesha katika mauti yake yenyewe, ni Mungu akituonyesha, kwamba Yeye ni Mungu, na Yeye atawapa hao shauku ya moyo Wake, moyo wao, watakaotembea kwa unyofu mbele Zake.

64 Tukiona jambo hili, ya kwamba Yeye ni Mungu, nasi sote hatuna budi kufikia mahali hapa, basi hebu tuangalie ishara Zake za madhihirisho. Upendo Wake, Kanisa Lake, watu Wake, na kila kitu kilicho, vyote ni madhihirisho ya Mungu kwetu. Basi ninafikiri sisi sote tunapaswa kuviinamisha vichwa vyetu katika unyenyekevu na kumshukuru Mungu kwa ajili ya maisha haya ambayo, kupitia kwa Kristo, yameshinda hata mauti yenyewe.

65 Na halafu Maneno ya Yesu wakati alipoenda kwa binti ya Yairo, "Hajafa huyu, bali amelala usingizi." Ameenda kulala usingizi, wala si kwa kifo chake. Kwa kuwa yeye alikufa miaka mingi iliyopita, kama msichana mdogo, na sasa anaishi katika

Kristo; naye amelala tu usingizi, kwetu sisi, bali ameamka pamoja na Kristo.

66 Na tuviinamishe vichwa vyetu basi na kutoa shukrani kwa ajili ya maisha haya hodari.

67 Baba wa Mbinguni, hakika Wewe unaijua mioyo yetu, hakika Wewe unayajua mawazo niani mwetu. Unajua yote kutuhusu. Sisi ni Uumbaji wa mkono Wako. Unajua tunasikitika kumwona Dada Bell ameondolewa kwetu. Lakini, Mungu, tunaviinamisha vichwa vyetu na mioyo, kwa shukrani kwamba ombi lake lilijibiwa, na kwamba shauku Yako kwake ilitimizwa. Kwamba, hata hapa kwenye mwisho wa safari, wakati tanzia yake imeandikwa katika maisha ya kila mtu aliyewasiliana naye, kwamba alikuwa ni mtumishi Wako. Ushawishi wake na udumu muda mrefu mioyoni mwa wote wanaomfahamu. Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utaipa raha nafsi yake hodari katika Nchi hiyo aliyoipenda, na kuzungumza habari zake na kuimba habari zake, miaka hii yote.

68 Ninamwombea Jimmy, alasiri ya leo, Bwana. Ninapomwona ameketi pale, naye anaonyesha mawazo yake huku machozi maangavu sana yakitiririka shavuni mwake. Yeye anawaza juu ya mke mtiifu. Na hawa watoto ambao, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao, wanawaza juu ya mama mpendwa. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawabariki. Ifariji mioyo yao. Unyoshe Mkono huo, ambao kupita panapoweza kufikiwa na kitu kingine chochote, unaoweza kuingia moyoni mwa mwanadamu, na uwape ridhaa hii kuu, ya kwamba siku moja tutakutana tena, nasi kamwe hatutafanya ibada nyingine ya mazishi Kule.

69 Wabariki wapendwa wake, ndugu zake, dada zake, wajukuu wake, na jirani zake.

70 Nayo makanisa haya, Bwana, tunajua jinsi yalivyompenda. Wakati alipotembea miongoni mwetu, wao, ametembea miongoni mwao. Na pamoja, pamoja nao, Bwana, tu—tunashiriki hisia hii yetu sote, ya kwamba tulimpenda. Nasi tupo hapa tukionyesha shukrani ze—ze—zetu Kwako, kwa ajili ya maisha yake.

71 Tufinyange, Bwana, na utufanye, kwamba sisi, pia, tutakapofika mwisho wa safari, tuwe tayari kukutana na Wewe. Samehe dhambi zetu nyingi, Ee Mungu wa Milele. Uturehemu, Bwana, kwa kuwa sisi ni dhaifu na wachovu.

72 Nami naomba ya kwamba Wewe utatufariji, alasiri ya leo. Jalia tuipate kwenye maneno haya ambayo yametamkwa kutoka kwenye Neno Lako, kupitia wahudumu mbalimbali, na hao waliokusudiwa kuyaleta hayo, na kupitia majirani na marafiki. Jalia tupate mle ndani, pamoja na ushuhuda wa—wa maua, na miti, na mwangaza wa jua, majani, na—na zaidi ya yote, pamoja na Uwepo wa Roho Mtakatifu, ambao hushuhudia kufufuka

Kwake Kristo. "Sitawaacha yatima. Nitamwomba Baba, na Yeye atawapa Mfariji mwingine, na Yeye atakaa milele." Loo, jinsi tunavyompenda, Bwana! Na jinsi tunavyokuthamini Wewe kumtuma Yeye kwetu, kutupa hakikisho hili lililobrikiwa katika majira na wakati wa shida.

Sasa tupe nguvu kwa ajili ya sehemu inayokuja ya ibada.

73 Ninataka kuomba maalum, Bwana, sasa hivi kwa ajili tu ya wavulana hawa wanaoketi hapa wamevaa nguo rasmi. Wabarikiwe wavulana hao, kwa kuwa itawabidi kurudi katika madaraja yao. Lakini ninaomba, Bwana, ya kwamba kwenye siku hiyo. . .Tunazithamini hizi nguo rasmi wanazovaa sasa. Lakini ombi la mama na lijibiwe: jalia wavikwe utakatifu na haki ya Yesu Kristo, kwenye siku ile. Hao wasichana, na wote pamoja, Bwana, hivyo ndivyo tunavyotaka kuwa, askari Wakristo, imani imara kweli. Tuongoze na utuelekeze mpaka siku hiyo, Bwana, tutakapokutana tena.

74 Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya maisha yake sasa, na tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nasi sote mpaka sote tutakapokutana miguuni Pako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

*MADHIHIRISHO* SWA62-0313
(Expressions)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne alasiri, tarehe 13 Machi, 1962, kwa ajili ya mazishi ya Dada Mary Bell katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org